



USAID/TANZANIA PUBLIC SECTOR
SYSTEMS STRENGTHENING ACTIVITY



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Machi 27, 2017

TOVUTI MPYA ZA SERIKALI KUBOresha USIMAMIZI NA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI

Sekretarieti za Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na Halmashauri zake 185, leo zimezindua tovuti zake mpya katika uzinduzi wa kitaifa, tukio lililofanyika mkoani Dodoma, mgeni rasmi akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. George Simbachawene. Uzinduzi huu uliweza kuonyesha muonekano mpya wa tovuti za serikali – mpangilio sanifu ambao utatumiwa na Mamlaka za Mikoa na Halmashauri nchini kote, ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumushi wa Umma, Mhe. Angela Kairuk, na Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, na Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID/Tanzania), Tim Donnay, pia walihudhuria.

Matumizi yenye ufanisi ya tovuti hizi yatachangia kuifanya Serikali kuwa wazi zaidi na yenye kuwajibika, pia itawezesha Serikali kuboresha huduma zake kwa wananchi. Kwa miaka mingi wananchi wamekuwa wakipoteza muda mwingi katika kona za Halmashauri zao wakihitaji taarifa, mathalan, jinsi ya kupata leseni ya biashara ama taarifa juu ya shule na vituo vya afya. Hata hivyo, maelezo na dashibodi zilizomo katika Tovuti zitatoa taarifa muhimu, hivyo kuokoa muda na kuiwezesha Serikali kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi wake.

Hili litafanikiwa kwa sehemu kubwa kwa kuboresha mawasiliano ya ndani kati ya mihimili inayotawala pamoja na mawasiliano na-umma. Mfano, tovuti hizi zitaimarisha utawala bora kwa kukuza jitihada za uwazi wa Serikali katika ngazi ya Kitiafa na Halmashauri, kwa kuwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikisha taarifa na nyaraka kwa wananchi na sekta binafsi. Tovuti pia zitaboresha usimamizi wa ndani na ufanisi kwa kuongeza urahisi wa upatikanaji wa taarifa, kuanzisha hifadhi ya taarifa za Halmashauri, kuboresha mawasiliano ndani ya Tawala za Mikoa na kati ya Serikali za Mitaa na kitaifa, na kuboresha taarifa za Serikali zinazoenda na wakati. Zaidi ya yote, tovuti zilizozinduliwa zitakuza matumizi ya taarifa, uwajibikaji, uwazi, ushiriki wa wananchi, tija na ufanisi.

Tovuti mpya za Serikali zimeundwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID). Juhudi hizi zinafanyika chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya sekta za Umma (PS3), Mradi wa miaka mitano unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID). Mradi huu uliundwa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Katika uzinduzi mkoani Dodoma, Mkurugenzi Msaidizi wa USAID/Tanzania, Tim Donnay, alieleza: “Umuhimu wa uzinduzi huu hauegemei katika kujenga ufanisi, uwazi na imani kwa wananchi pekee. Unaegemea pia katika umuhimu wa kuzipa mamlaka Halmashauri, pamoja na nguvu ya kufanya maamuzi.”



USAID/TANZANIA PUBLIC SECTOR
SYSTEMS STRENGTHENING ACTIVITY



Tovuti hizi mpya ni hatua muhimu sana katika muelekeo huu. Hii inaonyesha kujitoa kwa ugawanyishaji wa mamlaka kwa kuziruhusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutumia taarifa kujibu mahitaji ya wananchi

Uzinduzi huu wa Kitaifa ni muendelezo wa uzindizi wa tovuti za Tawala za Mikoa mitano na Halmashauri 37 kutoka Kanda ya Ziwa ambazo zilizinduliwa mwezi Februari. Kwa ushirikiano wa TAMISEMI, eGA na USAID, utekelezaji wa tovuti za Serikali unahakikisha kwamba Mikoa yote na Halmashauri zake zinapatiwa mifumo bora ya kushirikisha wananchi na kuboresha usimamizi.

###